



WOSIA



***Na Advocate
Harold Sungusia
Country Director
Sung Consultants***

www.sungconsultants.co.tz

Dondoo

1. Wosia ni Nini?
2. Wosia ni Muhimu?
3. Nani anaweza Kuandika Wosia?
4. Wosia unaweza kukubalika kisheria?
5. Nani warithi halali?
6. Mgonjwa Mahtuti aandikeje wosia?
7. Wosia Unahifadhiwaje?


Kielelezo - Wosia unafananaje?



1. Wosia ni Nini?

- Ni tamko la mdomo au maandishi anayotoa mtu wakati wa uhai wake kuelezea jinsi atakayotaka mwili wake utendewe na mali zake zigawanywe atakapokuwa amefariki.
- Wosia ni siri ambayo hufichuka wakati mtu aliyeutoa anapokuwa amefariki.





2. Kuna umuhimu gani wa kuandika wosia?

- Unaweka mambo yako bayana kuondoa utata kwa familia na jamii yako.
- Unamchagua msimamizi wa mirathi yako unayemtaka wewe.
- Unatoa maelezo juu ya mwili na mali yako kama upendavyo wewe na kwa mujibu wa sheria.

3. Nani anaweza kuandika wosia?

- Mtu yeyote [***Mume*** au ***Mke***] mwenye umri wa miaka 18 au zaidi na mwenye akili timamu.

Angalizo: “Kuandika wosia si uchuro bali ni kujizatiti katika kuhakikisha mambo yako ni sawa hata usipokuwapo.”

4. Wosia unaokubalika kisheria ni Upi?

- ✓ Wa maandishi au matamshi
- ✓ Uliosuhudiwa na watu wawili ikiwa ni wa maandishi na watu wanne ikiwa ni wa matamshi.
- ✓ Ni muhimu mmoja wa mashahidi awe ndugu wa karibu ila asiwe ni mrithi
- ✓ Wosia uwe ni wa mali zako binafsi na si mali za mtu mwingine
- ✓ Haikubailiki mtoa wosia kumnyima mrithi halali mali bila sababu zinazokubalika kisheria.

....4. Wosia unaokubalika kisheria ni Upi?

- ✓ Ushuhudiwe na mashahidi wasiopungua wawili kama mtoa WOSIA anajua kusoma na kuandika au wanne kama hajui kusoma na kuandika.
- ✓ Mmoja au wawili wa mashahidi lazima awe ndugu wa mtoa WOSIA.
- ✓ Mashahidi pamoja na Mtoa Wosia lazima waweke saini zao kwa wakati mmoja.
- ✓ WOSIA usitolewe katika mazingira ya kulazimisha au kushawishiwa.
- ✓ Kama ni WOSIA wa Kiislamu lazima uwe umefuata taratibu zote za WOSIA za Kiislamu kama kutorithisha zaidi ya theluthi moja ya mali kwa watu wa nje.

....4. Wosia unaokubalika kisheria ni Upi?

- ✓ WOSIA unatakiwa uwe na tarehe, mwezi na Mwaka ambao umeandikwa.
- ✓ WOSIA uwe umeandikwa kwa kalamu isiyofutika au kuchapwa na mashine.
- ✓ WOSIA unatakiwa kubatilisha WOSIA zote zilizopita.
- ✓ Wanufaikaji wanatakiwa kutokuwa mashahidi katika WOSIA.
- ✓ WOSIA haupaswi kuandikwa Kwa kufutwafutwa.
- ✓ Mtoa Wosia anaweza kutaja sehemu anayotaka azikwe



5. Nani ni Warithi halali wa kisheria?

- Mke/mume
- Watoto waliozaliwa ndani ya ndoa
- Watoto walio halalishwa kisheria[isipokuwa kwa Mirathi ya Kiislam]
- Wazazi na ndugu wa karibu waliokuwa wakimtegemea mtoa wosia wakati wa uhai wake.

5. Nani ni Warithi halali wa kisheria?



6. Mrithi anaweza kuachwa kwenye Wosia?

- Amezini na mke wa mtoa urithi,
- Amejariibu kumuua, amemshambulia, au amemduru vibaya mtoa urithi au mama mzazi wa mrithi,
- Bila sababu ya haki, hakumtunza mtoa wosia kutokana na njaa na ugonjwa,
- Ameharibu mali ya muusia, uharibifu wake utahesabika katika kukadiria kiwango cha urithi atakaostahili kupata.

6. Mrithi anaweza kuachwa kwenye Wosia?




6. Mrithi anaweza kuachwa kwenye Wosia?

- dini sio sababu ya kumnyima mrithi urithi.
- muusia akimnyima mrithi urithi wake, lazima ampe nafasi ya kujitetea mbele yake au Baraza la Ukoo, na lazima atoe sababu za kumnyima urithi.
- Lakini mrithi baada ya kujua amenyimwa urithi akikaa kimya bila ya kujitetea mbele ya mtoa urithi au Baraza la Ukoo, hawezi tena baadaye kupinga huo wosia.
- Kama mrithi hakuwa na habari za kunyimwa kwake urithi, atatoa malalamiko yake kwenye Baraza la Ukoo ambao watamsikiliza na wanao uwezo wa kukubali au kukataa.
- Ikibainika kwamba muusia alimnyima mrithi urithi kimakosa, wosia utabadilishwa na urithi utagawanywa kulingana na urithi usio na wosia.

7. Je, Ikiwa Mtoa Wosia Ni Mahtuti?

- Iwapo mwandika wosia ni mgonjwa mahututi ni muhimu ithibitishwe kuwa mtu huyo anaelewa anachokifanya na akili yake ni timamu wakati wa kuandika au kutamka wosia wake.



7. Je, Ikiwa Mtoa Wosia Ni Mahtuti?



`8. Wosia Unahifadhiwaje?

- Wosia uloandikwa unaweza kuhifadhiwa:-
 - A. RITA – Wakala wa Vizazi na Vifo – Kujaza Fomu mbili maalum
 - B. Kwa Wakili
 - C. Benki
 - D. Taasisi za kidini kama Kanisa au msikiti.
 - E. Kwa mtu yeyote ambaye si mrithi katika wosia huo na anaaminika kuwa ana uwezo wa kutunza siri.



Tahadhari

**KAMA BADO HUJAANDIKA WOSIA FANYA
HIVYO LEO**

CHUKUA TAHADHARI WAKATI UNGALI HAI!!

Mhubiri 8:8(a)

Yeye ajuae lililo la haki asilifanye huyo atenda
dhambi

Mfano wa Wosia

Maelekezo

1. Huu ni wosia wangu wa mwisho mimi

.....

S. L. P.....

2. Namchagua.....

S. L. P.....

Simu:.....

Ambaye anaishi.....

Kuwa msimaizi wa mirathi yangu.

3. Nitakapokufa mwili wangu ukazikwe:.....

.....

Wilaya.....

Mkoa:.....

4. Mali zangu/yangu ni:.....

.....

.5. Natamka kwamba mali zangu zote zinazohamishika na
zisizohamishika zitamilikiwa na ke/mume wangu aitwaye

.....

Iwapo atakuwa hai baada ya kufa kwangu

6. Iwapo mke/mume wangu aitwaye.....

Atafariki mapema kuliko mimi, mali zangu zitarithiwa na watoto
wangu wafuatao:-

a)

S. L. P.:..... Simu:.....

b)

S. L. P.:..... Simu:.....

c)

S. L. P.:..... Simu:.....

Katika mafungu yaliyo sawa sawa
imetiwa sahihi hapa.....

.....siku ya.....

Mwezi wa.....

Mwaka.....

Sahihi ya Mtoa Wosia

Mbele ya Mashahidi:-

1.....

2.....

3.....

Mshuhudi Majinasahihi

MBELE YANGU

Jina la Wakili:.....

Sahihi:.....Muhuri.....

Anuani:.....Cheo.....

Hitimisho

- 1 Timotheo 6:6-10
- James 1:27 Pure religion and undefiled before our God and Father is this: **to visit the fatherless and widows in their affliction, and to keep oneself unstained by the world.**

Yakobo 4:17

Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi,
kwake huyo ni dhambi.

- Proverbs 13:22 ¶A good man leaveth an inheritance to his children's children: and the wealth of the sinner is laid up for the just.
- Proverbs 19:14 ¶House and riches are the inheritance of fathers: and a prudent wife is from the LORD.
- Proverbs 20:21 ¶An inheritance may be gotten hastily at the beginning; but the end thereof shall not be blessed.
- Luke 12:13 ¶And one of the company said unto him, Master, speak to my brother, that he divide the inheritance with me.